TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO WA SABA WA WADAU WA KAHAWA, 2016.

NA	AZIMIO	MHUSIKA	UTEKELEZAJI
1	Kuwepo na mikakati ya kutatua changamoto za masoko ya kahawa yenye lengo la kuongeza ushindani kwenye soko la kahawa; kuimarisha soko la ndani na kumsaidia mkulima kupata bei nzuri.	TCB	Mikakati na shughuli mbalimbali za kutatua changamoto za masoko ya kahawa nchini zimefanyika ikiwa ni pamoja na ifuatayo; I. Kutangaza kahawa ya Tanzania kimataifa ambapo Tanzania ilishiriki katika maonyesho ya kimataifa ya kahawa bora – AFCA yanayofanyika kila mwaka, katika mwaka 2017 yalifanyika Addis Ababa Ethiopia. II. Juhudi za usindikaji wa kahawa kwa ajili ya soko la ndani na usafirishaji nje zimeongezeka ambapo katika mwaka 2017 jumla ya kampuni 26 zilipata leseni za usindikaji na ziliendesha shunguli za usindikaji wa kahawa. III. Bodi ya kahawa imendelea kuwatambua na kutoa mafunzo kwa wauzaji kahawa wa mitaani (Ghahawa) na katika mwaka huu wa fedha mafunzo yalifanyika katika mikoa ya Tanga na Manyara IV. Serikali imefuta ada ya leseni ya uchakataji na usindikaji kahawa kiasi cha dola za kimarekani 250 ili kutoa motisha wa kuongeza kiasi cha kahawa inayosindikwa na kuchakatwa katika CPU V. Bodi ya kahawa imeendelea kutoa bei dira ya kahawa na kuisambaza kwa njia ya mitandao ya simu ili kumsaidia mkulima pale anapofanya uamuzi wa kuuza kahawa yake Bei lelekezi inapatika kwakutuka ujumbe **“kahawa bei” kwenda no 15550** VI. Bodi inaendelea na mkakati wa kuboresha uendeshaji wa mnada wa kahawa ambapo lengo ni kubadili (Upgrading) mashine ya kuendeshea mnada wa kahawa ili kuwezesha wanunuzi wa kahawa kushiriki kwenye mnada bila ya kuwalazimu kuwepo kwenye chumba cha mnada (Remote bidding). Mpango huu utakapokamilika utawezesha kuongezeka kwa wanunuzi wa kahawa mnadani kwa wakati mmoja hivyo kuongeza ushindani. Tayari andiko la kuomba fedha za kutekeleza mpango huu limetayarishwa na kuwasilishwa kwa wafadhili na pindi fedha zitakapopatikana mpango huu utatekelezwa mara moja.
2	TaCRI ishirikiane na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kufuatilia upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya utafiti wa kahawa katika Wilaya ya Tarime-Mara na Buhigwe-Kigoma.	TaCRI, LGAs, TCB	▪ Hatua nzuri imefikiwa na halmashauri ya wilaya Tarime wamekubali kutoa ekari 10 katika kijiji cha Borega A. Lengo ni kufikisha ekari 30. ▪ DC Buhigwe ataitisha kikao cha uhalalishaji wa ardhi ya Mwayaya kwa TaCRI katika tarehe itakayo pangwa.

3	Serikali kupitia Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi itimize ahadi yake ya kuchangia shilingi bilioni mbili kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kahawa ambayo haijatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita.	WKMU, TCDF, TCB	Taarifa ya utekelezaji wa azimio hili itawasilishwa katika taarifa ya TCDF katika mkutano huu.
4	Kuwepo na mkakati wa kuhamasisha matumizi ya mbolea, kuanzisha mashamba darasa ya matumizi sahihi ya mbolea na kuimarisha huduma za ugani.	LGAs, TCDF	Katika msimu huu mfuko wa maendeleo ya kahawa ulianza kwa kutoa ruzuku asilimia hamsini ya bei kwa ya miche ya kahawa ili kutoa nafuu ya bei kwa miche kwa wakulima na kuhamasisha upandaji wa miche bora. Mpango wa kuhamasisha matumizi ya mbolea utaanzishwa sambamba na mpango wa kuwawezesha wakulima pembejeo pale utakapoanza.
5	Serikali iendelee kutoa ruzuku kwenye zao la kahawa	WKMU	Serikali imeendelea kutoa ruzuku kwa sekta ya kahawa katika maeneo yafuatayo: - Kughamia Bodi ya kahawa Tanzania - Kutoa ruzuku ya uzalishaji wa miche ya kahawa kwa taasisi ya utafiti wa kahawa Tanzania (TaCRI) - Kugharamia shughuli za ugani zinazondeshwa na Halmashauri za wilaya
6	Benki ya Maendeleo ya Kilimo ianze kutoa huduma za mikopo kwenye zao la kahawa kama inavyofanya kwenye mazao mengine na ialikwe kuhudhuria mkutano ujao wa wadau.	TCB, TADB,	Benki ya kilimo ilialikwa kushiriki mkutano huu na imeombwa kutoa wasilisho juu ya huduma zake kwenye sekta ya kahawa.
7	Randama ya Makubaliano ya wadau ya mwaka 2011 ifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia mapendekezo yaliyowasilishwa kwa kuzingatia viwango vya uchangiaji vilivyokubalika awali. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo: Utafiti – 0.75%, Mfuko – 0.2%, Mnada wa kahawa – 0.2%.	TCB, TCDF, WKMU, TaCRI	Randama hii ilikamilika ila haikusainiwa na wahusika kwa kuwa inatarajiwa kufanyiwa tena marekebisho baada ya mkutano huu,kutokana na matarajio ya mabadiliko ya viwango vya uchangiaji yatakayotokana na maelekezo ya serikali.
8	Mapendekezo ya wadau ya kuongeza viwango vya uchangiaji katika Mfuko, Utafiti na Bodi yafanyike baada ya utekelezaji wa tamko la Serikali la kupunguza kodi na makato katika tasnia ya kahawa, na kwa utaratibu maalumu utakaokubaliwa na wadau kwa kuitisha mkutano mkuu maalumu kusaini randama ya makubaliano.	TCB, TCDF, WKMU, TaCRI	Utekelezaji wa tamko la serikali kupunguza kodi na makato katika sekta ya kahawa litatolewa katika mkutano huu.
9	Kuwepo na mikakati mahususi ya kuwezesha vijana kushiriki katika mnyororo wa thamani wa zao la kahawa.	TCB, LGAs	I. Bodi ya kahawa kwa kushirikiana na chuo kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) wameanzisha mafunzo ya ngazi ya cheti katika ubora wa kahawa na biashara (*Coffee quality and Trade*) ili kupunguza pengo la wataalam wa ubora wa kahawa

			na masoko lililoko kwenye sekta ya kahawa na kufanya sekta hii kutegemea wataalam hawa kutoka nchi za jirani. Mpango huu ulianzishwa miaka miwili iliyopita na vijana wahitimu wa kozi hii wameajiriwa katika maeneo mabalimbali ya sekta ya kahawa. II. Baadhi ya Halmashauri za wilaya zimeanzisha mifuko ya vijana na kinamama ambapo vijana wamepewa mikopo iliyowawezesha kuanzisha shunguli mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa kahawa. Mf. H/w Moshi, Hai.
10	Sheria ya Tasnia ya Kahawa ifanyiwe marekebisho kuruhusu wakulima wa kahawa kuuza kahawa ya madaraja yote nje ya nchi.	TCB, WKMU, TCDF	Azimio hili halikutekelezwa kwa kuwa kanuni zilizopo zinazoruhusu kahawa za ubora wa juu na madaraja ya juu pekee kuuzwa kwa utaraibu wa moja kwa moja (Direct export). Bodi ya kahawa kama msimamizi wa sekta ya kahawa bado ina maoni kuwa utaratibu huu bado una maslahi kwa sekta ya kahawa na Taifa kwa ujumla.
11	Mpango wa Mfuko wa kuwawezesha wakulima kupata mbolea (Pembejeo) uboreshwe kwa kuzingatia maoni na mapendekezo ya wadau kabla ya kuanza kutekelezwa.	TCDF, WKMU	Mpango huu uliboreshwa kulinga na maoni ya yaliyotolewa katika mkutano uliopita. Utekelezaji wake utaanza msimu ujao wa uzalishaji wa kahawa 2017/2018 kwa majaribio (Taarifaa ya ufafanuzi itatolewa katika mkutano huu katika na TCDF).
12	Maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo cha kahawa yabainishwe, yapimwe hati miliki zitolewe na masharti ya uendelezaji yasimamiwe.	TCB, WKMU, LGAs, ARDHI	Halmashauri za wilaya zilinazolima kahawa ziliwasilisha bodi ya kahawa kiasi cha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha kahawa ikiwa ni hatua ya awali ya kuyatambua. Taarifa ya maeneo hayo imeambatanishwa ***(Kiambatisho Na. 1)***
13	Wadau wa kahawa watekeleze mkakati waliojiwekea wa kuzalisha miche milioni 20 kwa mwaka na kuhakikisha kwamba kila mkulima anapanda miche mipya.	TCB, TaCRI, LGAs	TaCRI kwa kushirikiana na wadau wote imezalisha na kusambaza miche 2,220,188 kati ya matarajio ya kuzalisha miche 5,000,000. Ukosefu wa fedha ni changamoto katika kuzalisha miche. Tunatarajia kuwa ifikapo mwezi wa sita mwishoni, idadi itafika milioni tatu (3,000,000) kwani baadhi ya miche bado iko kwenye masanduku ya kukomazia Pia halmashauri mbalimbali zinazolima kahawa nchini zimewezesha wakulima kuzalisha kupata miche ya kahawa kupitia utaratibu wa utekelezaji wa shunguliza maendeleo ya kilimo ***(Kiambatanisho No 2)***
14	Serikali iweke mazingira mazuri ya kuendeleza sekta ya kahawa.	WKMU, TCB, LGAs, WVB	Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya biashara katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la kuboresha mazingira ya udhibiti na utoaji leseni. Bodi ya kahawa na taasisi nyingine za uthibiti (Regulatory Agencies) nchini zimeshirikishwa katika mchakato wa kutayarisha mapendekezo ya mageuzi (reforms) ya kuboresha mazingira ya utoaji leseni na udhibiti unaoendelea chini ya wizara ya viwanda na biashara. Matarajio ni kuwa mageuzi haya yatakapokamilika yataboresha mazingira ya biashara na kuendeleza sekta ya kahawa nchini.